**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

### Kikao cha Kwanza

*(Mkutano wa Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

### WIMBO WA TAIFA

*(Hapa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa)*

### DUA

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

### HATI ILIYOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. PHILIP S. MARMO):**

Nakala za Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

**SPIKA:** Ahsante sana. Kuna tatizo la kipaza sauti hapo, Mheshimiwa Waziri hakusikika vizuri, naomba kirekebishwe hicho.

Waheshimiwa Wabunge, karibuni Dodoma kwa Mkutano huu wa Kumi na Mbili. Natumaini wote mmesafiri salama. Tunaendelea na kazi yetu hii ambayo kidogo itakuwa ndefu hadi tarehe 29/8/2008.

Swali la kwanza asubuhi hii linaulizwa na Mheshimiwa Idd Azzan, Mbunge wa Kinondoni na linaelekezwa Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

### MASWALI NA MAJIBU

Na. 1

## Ukosefu wa Mifereji ya Kuondoa Maji ya Mvua Barabarani Jimbo la Kinondoni

**MHE. IDD M. AZZAN** aliuliza:-

Kwa kuwa mvua kubwa zilizonyesha mwaka huu (2008) Mkoani Dar es Salaam zimesababisha mafuriko makubwa kwenye Jimbo la Kinondoni kutokana na kukosekana kwa mifereji ya kuondoa maji kwenye barabara zilizoko kwenye Kata ya Mwananyamala, Makumbusho, Kinondoni, Tandale na Hananasif; na kwa kuwa fedha za Halmashauri ya Konondoni zinatokana na vyanzo vyake vya mapato pamoja na ruzuku kutoka Serikali Kuu ambazo hazikidhi kuondoa kero hiyo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia Halmashauri hiyo ili kuondoa kero na adha kubwa wanayoipata wananchi wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa sana, ninakuomba, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Azzan, nitoe maneno macheche sana yanayofuatana na uteuzi wangu.

Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha hapa aliponifikisha.

Nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa heshima kubwa sana aliyonipa mimi na heshima ambayo ameitoa kwa wananchi wangu wa Jimbo la Siha.

Ninachoweza kusema katika mkutano huu ni kwamba nitamsaidia Rais, nitamsaidia Waziri Mkuu, Mawaziri na Wabunge wenzangu kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue pia fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Siha kwa kunichagua na kuwa Mbunge wao. Nisingefika hapa kama wasingefanya uamuzi walioufanya.

Kipekee pia naishukuru familia yangu, mke wangu Grace na watoto pamoja na mama yangu mzazi. Nawashukuru sana na Mungu awabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nawashukuru Wabunge wote ambao mlinitakia kheri, Spika wewe mwenyewe ulikuja siku ya kuapa na Mawaziri wengine pia walikuja. Nawashukuru kwa meseji mlizoniletea, Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sauti hii itaendelea kupanda, naomba mnisamehe, ikipanda ni kama kawaida. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kujibu swali la Mheshimiwa Idd Azzan, Mbunge wa Kinondoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba mvua kubwa zilizonyesha mwaka huu Mkoani Dar es Salaam, zilisababisha mafuriko sehemu mbalimbali za Jiji ikiwemo Jimbo la Kinondoni. Mafuriko kwenye Jimbo la Kinondoni yalisababishwa na baadhi ya barabara kutokuwa a mirefeji ya maji ya mvua na kuwepo kwa miundombinu ya maji ya mvua chini kwa chini yaani *underground drainage channels* ambayo ilijengwa mwaka 1950 hasa maeneo ya Mwananyamala na Kinondoni ambayo sasa imechakaa na kuzidiwa na uwezo. Pia kuna maeneo korofi yanayojaa maji na kusababisha mafuriko makubwa, kwa mfano Bwawa la Msisiri "A" na *Shoppers Plaza*; kwa kuwa ni maeneo asili ya kutawanya maji ambayo kwa sasa yameendelezwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile pamoja na baadhi ya maeneo kuwa na mifereji ya maji ya mvua kwa mfano Tandale, mifereji hiyo imekuwa haiwezi kukidhi utiririkaji na usafirishaji wa maji ya mvua. Kwa hiyo, kuhitaji upanuzi baada ya *catchments area* kuendelezwa.

Aidha, sababu nyingine inayochangia kuwepo kwa mafuriko, ni mikondo asili ya maji ya mvua kubadilishwa kuwa viwanja na wananchi kuvamia mikondo ya asili na kujenga nyumba hususani eneo la bonde la mpunga Msasani.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na tatizo hili, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imefanya juhudi zifuatazo:-

(i) Katika bajeti ya mwaka 2007/2008, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ilipeleka fedha wastani wa Shilingi 100,000 – 300,000 kwa Kata 16 kwa ajili ya kusafisha mifereji ya maji ya mvua iliyopo katika Kata hizo kwa Mpango Shirikishi Jamii.

(ii) Katika bajeti ya matengenezo ya barabara mwaka 2008/2009, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imeomba kupatiwa kiasi cha shilingi milioni 491 kwa ajili ya kujenga mifereji mipya ya maji ya mvua katika maeneo korofi. Maeneo yatakayohusika ni pamoja na Makumbusho, Mwananyamala, Kinondoni na Msasani.

(iii)Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni pia ina mikakati ya upanuzi wa mifereji ya maji ya mvua eneo la Tandale Kwamtogole, ukarabati na uzibuaji wa mifereji ya maji ya mvua na makalvati maeneo ya Hananasif, Mwananyamala na Kinondoni, ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua katika shule mpya za Sekondari mfano Shule ya Turiani na Kijitonyama.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri na nimpongeze kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salaam ndiyo kitovu cha nchi yetu, hali ya miundombinu ya Dar es Salaam inasikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, ili Jiji hili liweze kufanikiwa, Serikali na Halmashauri haziwezi kwa vyanzo vyake, je, Serikali iko tayari kuziruhusu Halmashauri ziweze kukopa ili tuweze kubadilisha miundombinu hii?

Mheshimiwa Spika, kuna mfereji wa Bungoni, katika mvua hizi za karibuni watu kwa muda wa wiki mbili walikuwa hawalali, walikuwa wanasimama vyumbani mwao, unaweza kuona taabu na kero wanazozipata. Sasa naiomba Serikali ituruhusu Halmashauri tuweze kukopa na tukikopa thamani ya nyumba hizi zitapanda juu na zitaweza kuongeza tena kodi ya majengo ili ku-*service* mkopo huu.

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri! Kuna swali na ushauri humohumo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, *concern* ambayo inaletwa hapa kuhusu Jiji la Dar es Salaam ni *concern* ya kila mtu na hasa wale wanaoishi Dar es Salaam na ni *concern* pia ya Serikali. Sisi wote tunafahamu kabisa kwamba mvua ziliponyesha Dar es Salaam hali ile ilikuwa ni hali ya kusikitisha. Kwa hiyo, nadhani muuliza swali, Mbunge mwenzegu hapa ana-*address* suala ambalo ni *pertinent* na ambalo kwa kweli hakuna ubishi wowote kwamba hali ya Dar es Salaam si nzuri, hii hatuhitaji kueleza sana bali tunahitaji tu *effort* kidogo tu ya kuelewa ni nini kinachozungumzwa.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi anapendekeza suala la Halmashauri ziweze kuruhusiwa kukopa. Ndani ya mfumo wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, uko utaratibu wa kwetu sisi humu humu ndani, unaoruhusu Halmashauri kukopa katika mfuko wa kwetu ambao unatokana na Halmashauri yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo, ni jambo ambalo linakubalika kabisa kwamba kama Halmashauri tumefika mahali tukaona kwamba kuna tatizo kubwa kiasi hiki na iko shabaha ya kuona kwamba tukope mahali pengine, naamini Serikali itakuwa tayari kuzungumza na kuona uwezekano wa kufanya hivyo. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la Dar es Salaam na mlundikano wa maji machafu, si suala la utanuzi wa mifereji tu. Je, Mheshimiwa Waziri atatueleza nini kuhusu *feeder road* au njia za vichochoroni ambazo matofali ya udongo yanapatikana kwa wingi Tanzania lakini Halmashauri ya Jiji imeshindwa hata kutengeneza zile barabara na wameshindwa hata kuweka *dustbin* na kusababisha uchafu kuingia kwenye hiyo mifereji na kufanya izibe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu la Mheshimiwa Mnyaa kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa katika kufuatilia jibu la swali hili, yapo mambo mengi sana ambayo yanatokea katika jiji la Dar es Salaam na ninajua pia inatokea katika Miji mingine katika Tanzania. Hizi *feeder roads* ambazo amezizungumzia, ni kweli kwamba tungeweza tukatumia matofali haya ya kuchoma. Kinachoonekana Dar es Salaam sasa hivi, ni zaidi ya hiyo.

Kama nilivyoeleza hapa, mfumo ule uko hoi, umekaa pale toka mwaka 1950, ni miaka mingi sana. Kwa hiyo, utaona kwamba hata suala linalozungumziwa la *dustbin* kwamba hakuna na kadhalika, ni suala ambalo linarudi katika Manispaa zenyewe kwa maana ya Manispaa ya Kinondoni. Hakuna tatizo lolote lile kutumia matofali haya ambayo yanazungumzwa hapa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba zile *feeder roads* zinawekwa katika hali nzuri.

Mheshimiwa Spika, tatizo tulilonalo pale, ni kwamba wananchi wote wale wanatakiwa waingizwe katika utaratibu shirikishi ili kuhakikisha kwamba wao wenyewe wanasafisha mifereji ile na kuhakikisha kwamba kila wakati inakuwa misafi na pia kuhakikisha kwamba hawachukui chupa na takataka wakatupa katika mifereji hiyo na kusababisha maji kusimama pale. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo, tuna hakika kwamba tutaliweka Jiji letu la Dar es Salaam katika hali nzuri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali la mwisho la nyongeza, Mheshimiwa Kaboyonga.

**MHE. SIRAJU JUMA KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa maana ya kufuatilia suala hili.

Mheshimiwa Spika, katika nchi nyingi duniani, miongoni mwa hati fungate (*bonds*) za muda mrefu zinazotolewa, ni pamoja na *Manispaa Bond*. Tanzania hatuna hati hizo lakini Dar es Salaam ni mji ambao unaweza kabisa kukopa kwa kutumia *Manispaa Bonds* na kwa maana hiyo na miji mingine yote.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali isiruhusu kwa kuanzia na Dar es Salaam itoe *Manispaa Bonds?*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nafikiri swali la Mheshimiwa Kaboyonga, ni swali zuri kabisa na hii yote inaonyesha *seriousness of the disease* kwamba *problem* ni kubwa na kila mtu amejaribu kuona kwamba ni njia gani ambayo inaweza ikatusaidia katika jambo hili. Sidhani kama nitakuwa ninai-*contradict* Serikali kwa kusema kwamba tutazingatia jambo hili na kuangalia jinsi ambavyo tunaweza kulifanyia kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba radhi kidogo kwamba nina tatizo la mafua. Lakini nimesimama kutaka kuongeza kidogo maelezo juu ya majibu

mazuri sana ambayo yametolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri na mimi nataka nimpongeze kwa dhati, umeanza vizuri, jitahidi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la Jiji la Dar es Salaam, nadhani linahitaji *attention* kubwa zaidi kwa upande wa Serikali. Juzi nilipokutana na Madiwani, niliahidi kwamba itabidi jambo hili tulirejeshe Serikalini ili tulitazame kwa pamoja. Hatuwezi kuendeleza Jiji la Dar es Salaam katika mazingira haya kwa kutegemea Manispaa peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zoezi hilo tumeanza kulifanyia kazi ili tuweze kuona tunafanyaje. Si masuala ya mifereji tu lakini kuna matatizo makubwa zaidi hata ujenzi wa majengo bali na mambo mengi chungu nzima.

Katika zoezi hilo, nimeona niunganishe vilevile na Manispaa ya Dodoma, kwa kuwa ni eneo ambalo linawiana sana na Jiji letu la Dar es Salaam.

Kwa hiyo, nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tupate nafasi kidogo baadaye tuje tueleze tumefanya nini katika kujipanga vizuri ili kuona kwamba Jiji la Dar es Salaam litasaidiwaje na Serikali katika mambo yote yale makubwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tunaendelea sasa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, swali linaulizwa na Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini, kwa niaba yake Mheshiwa Michael Lekule Laizer.

Na. 2

**Sheria ya Pensheni**

**MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER (K.n.y. MHE. OMARI S. KWAANGW')** aliuliza:-

Kwa kuwa Sheria ya Pensheni ilitungwa tangu enzi za ukoloni – *Pension Ordinance of 1954*:-

(a) Je, ni mabadiliko gani muhimu yamefanyika kwa makundi mbalimbali ya watumishi wa umma hadi sasa?

(b) Je, kwa sasa bado tuna kundi la watumishi wastaafu wanaolipwa Sh.21,601/= kwa mwezi na kama lipo linajumuisha wastaafu wa ngazi zipi?

(c) Je, wastaafu kuanzia mwaka 1965 hadi tarehe 30/6/1999, waliokuwa chini ya Sheria ya Pensheni ya mwaka 1954, walifaidika vipi na Sheria Namba 2 ya mwaka 1999 ikilinganishwa na wale waliostaafu kwenye miaka ya 1980?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Omari Shabani Kwaangw', lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mabadiliko muhimu yaliyofanyika kuhusu pensheni tangu Sheria ya Pensheni ilipotungwa enzi za ukoloni mnamo mwaka 1954 kwa makundi mbalimbali ya Watumishi wa Umma hadi sasa ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuruhusu malipo ya pensheni kufanyika kwa kujumuisha muda wa utumishi katika mashirika na ule wa Serikali kwa Watumishi wa Serikali walioajiriwa katika masharti ya pensheni wanaohamishiwa kwenye mashirika ya umma na watumishi wa kwenye mashirika ya Umma, wenye masharti ya *PPF*, wanaohamishiwa kwenye Utumishi wa Serikali kwenye ngazi zenye masharti ya pensheni ambao utumishi wao wa mashirika au Serikali (*qualifying period*) ulikuwa hauwapi sifa ya kulipwa pensheni wakati wa kustaafu.

(ii) Kubadili fomula ya kukokotoa hesabu za pensheni (*Pension Factor*) kwa madhumuni ya kumuongezea kipato mstaafu kutoka dinomineta ya moja ya mia sita (*one-sixth hundred*) ya mshahara wake wa pensheni kwa kila mwezi mtumishi aliofanyia kazi katika ajira ya masharti ya pensheni kuwa moja ya mia tano arobaini (*one-five hundred and forty*) ya mshahara wake wa pensheni kwa kila mwezi aliofanya kazi katika ajira ya masharti ya pensheni.

(iii) Kuongezeka kwa miaka inayohesabika kukokotoa kiinua mgongo cha pensheni (*Commuted Pension Gratuity*) toka kumi na mbili na nusu ($12^1/_2$) ya awali hadi kumi na tano na nusu (15½) kuanzia tarehe 1/4/1991.

(iv) Kubadili Mfuko wa Pensheni kwa watumishi wa Serikali za Mitaa kutoka *Provident Fund* na kuwa *Pension Fund* kwa kufuta Sheria Na. 6 ya mwaka 2000 ya *Local Authority Provident Fund* na kutungwa Sheria Na. 9 ya mwaka 2006 ya *Local Authority Pension Fund*.

(v) Kumpatia Rais wa Jamhuri ya Muungano mamlaka ya kumsamehe mtumishi sharti lolote lililoko katika Sheria iwapo sharti hili litafanya mtumishi kukosa pensheni bila sababu za msingi. Kwa mfano, kukosekana kwa moja ya kumbukumbu zinazohitajika katika kumlipa mtumishi pensheni.

(vi) Kutungwa kwa Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Kazi katika Utumishi wa Umma Na. 2 ya mwaka 1999, iliyoanza kutumika tarehe 1 Julai, 1999.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii ilifuta Sheria ya Pensheni, Sura 371 ya mwaka 1954 na ilianzisha utaratibu wa Watumishi wa Umma wanaoajiriwa kwa masharti ya Pensheni kuwa wanachama wa Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma *(PSPF)*, ambao wanachama na waajiri wao, huchangia Mfuko huo kwa ajili ya pensheni zao na watumishi wanachama kulipwa pesheni zao moja kwa moja na Mfuko huo wanaopostafu.

(vii) Umri wa chini wa kustaafu kwa hiari umeongezwa kutoka miaka 50 ya zamani kuwa 55 na umri wa juu kabisa wa kustaafu kwa lazima toka miaka 55 ya awali hadi miaka sitini (60).

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa bado wapo watumishi wastaafu wanaolipwa pensheni ya Sh.21,601/= kwa mwezi na hii ni baada ya kuongeza mara kwa mara kima cha chini cha malipo ya pensheni kama nilivyotaja hapa juu. Hata hivyo, ni vigumu kujua ni wastaafu wa kundi gani wanaolipwa kiasi hicho kwa kuwa kundi hilo linajumuisha wastaafu wa ngazi mbalimbali ambao walikuwa chini ya kima husika. Katika kupandisha kima cha chini cha pensheni, huwa haijalishi mhusika alistaafu kwa ngazi gani, kwani wastaafu wengi wa ngazi mbalimbali hujikuta wamerundikwa katika kundi moja baada ya ongezeko la kima cha chini cha pensheni kadri miaka inavyokwenda na mabadiliko kufanyika.

(c) Wastaafu kuanzia mwaka 1965 hadi tarehe 30 Juni, 1999, walikuwa chini ya Sheria ya Pensheni ya mwaka 1954, hawakufaidika moja kwa moja na Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Kazi katika Utumishi wa Umma Na. 2 ya mwaka 1999 kwa kuwa Sheria hii ilianza kutumika tarehe 1 Julai, 1999 na hivyo inawahusu watumishi wanaostaafu baada ya tarehe hiyo. Sheria hiyo haikujumuisha waliostaafu baada ya tarehe hiyo. Sheria hiyo haikujumisha waliostaafu kabla ya hapo ambao kwa mujibu wa Sheria husika hawawezi kuwa wanachama wa mfuko unaohusika.

**MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa pensheni ya Sh.21,000/= imepitwa na wakati, ni hela ndogo sana, je, Serikali haiwezi kuwasaidia wastaafu hawa kwa kupandisha pensheni ili iwe kima cha chini cha mshahara wa sasa ili iweze kuwasaidia watumishi hawa wanapostaafu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, sasa hivi Serikali inafanyia kazi na iko katika mchakato wa kuona uwezekano wa kuongeza kima cha chini cha pensheni. Kwa hiyo, naomba awe na subira tu wakati tukiendelea na shughuli hiyo.

**MHE. MWANAWETU SAID ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nina swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa wapo wafanyakazi ambao wamestaafu wakiwa wame-*graduate* na kwa kuwa wastaafu hao katika ngazi yao ambayo wame-*graduate* nayo wengine walikuwa ni TGS3 na mpaka wamefika hatua ya kustaafu wamefanya kazi miaka kadhaa na kwa kuwa walipoomba kutaka kuongezewa kutokana na ngazi yao, hawakuweza kufanikiwa kwa sababu waliambiwa kuna ushindani wa kuajiriwa na kwa kuwa watu hao wapo na sasa hivi wamestaafu wakiwa na TGS3 au chini ya hapo lakini ni *graduate.* Sasa hivi wapo ambao wame-*graduate* wana ngazi ya juu zaidi; je, Mheshimiwa Waziri

atatusaidiaje ili hawa watu waweze kupata haki yao ya pensheni kulingana na ngazi ambayo walitakiwa wawepo sasa hivi kwa sababu mpaka sasa hivi wako kwenye ngazi ya chini?

**SPIKA:** Swali hili halikueleweka vizuri na ninaona ni mahususi, labda muonane ili liweze kupata majibu ya uhakika zaidi. (*Makofi*)

Tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 3

**Wataalamu wa Fani Mbalimbali Waliostaafu**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Kwa kuwa, watalaamu wa fani mbalimbali ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi; na kwa kuwa, wapo watalaamu wengi ambao wameshastaafu kutokana na umri lakini elimu waliyonayo bado haijastaafu:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwaajiri wataalamu hao kimkataba ili waendelee kutoa utaalamu wao kwa maendeleo ya nchi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Viti Maalumu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 17 cha Sheria ya Pensioni kwa Watumishi wa Umma *(The Public Service Pension Act)* Na.2 ya mwaka 1999, umri wa kustaafu kwa lazima kwa Watumishi wa Umma ni miaka 60. Pamoja na masharti haya ya kisheria, Serikali pia imekuwa ikitoa miongozo ya mara kwa mara kuhusu umuhimu wa watumishi wa umma kustaafu kazi mara wanapotimiza umri wa kustaafu.

Mheshimiwa Spika, miongozo hiyo ni pamoja na Kanuni Na. D.22 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, Toleo la mwaka 1994 na pia Kifungu Na.11 cha Waraka wa Rais Na.1 wa mwaka 1992 na Kifungu Na. 12 cha Waraka wa Rais Na.1 wa Mwaka 1998. Kwa mujibu wa miongozo hii, watumishi wanaohitimisha ajira zao baada ya kufikia umri wa kustaafu kwa lazima, wanashauriwa kupumzika na kutumia uzoefu wao kwa kujihusisha na masuala mengine ya maendeleo ya jamii japokuwa wengine wanaweza kuitumikia Serikali kwa njia moja ama nyingine. Kutokana na hali hii, Serikali imeendelea kuajiri kwa mkataba watumishi waliofikia umri wa kustaafu pale inapoonekana kuna umuhimu wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutilia maanani upungufu wa wataalamu uliopo katika soko la ajira, Serikali imeendelea kuwaajiri baadhi ya wataalam wa sekta ya elimu, afya na Mahakama kwa masharti ya mkataba hadi hapo Taifa litakapojitosheleza kwa kuwa na wataalamu wanaohitajika.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kumuuliza swali moja.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika Bunge letu hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuna Wabunge mbalimbali ambao na wao pia wana fani mbalimbali za kiutalaamu kama *professors*, madaktari, *engineers*, wachumi, wanasheria na kadhalika ingawa wao ni wanasiasa, je, Serikali inawatumiaje Wabunge hawa ambao ni wataalamu wa fani mbalimbali?

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Waziri! Ni swali la kujipatia kipato cha ziada hili. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kidogo tukitoka hapa itabidi nielewane naye kwamba tuwatumie wakiwa tayari Wabunge au baada ya kuacha Ubunge kwa sababu sikulipata vizuri, kwa sababu kama wakiwa Wabunge kidogo inanisumbua kwa sababu sijui wataugawa vipi muda wao.

Lakini hata hivyo Watumishi wa Umma wanatakiwa wastaafu wanapoamua kuingia katika siasa hasa katika mfumo wa vyama vingi vya siasa. Kwa hiyo, kidogo tutakaa pembeni, tutaeleweshana jinsi ambavyo yeye anataka tuwatumie hawa Waheshimiwa Wabunge lakini kwa maana ya kujitolea, hatuwakatalii. *(Kicheko)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri kama ifuatavyo:-

Miongoni mwa wastaafu ambao wanastaafu wakiwa na umri mdogo ni Askari kulingana na mikataba yao na kwa sababu ya hali halisi ya maisha, wengi wao baada ya kufika muda wa kustaafu hupenda kuongeza muda lakini inaonekana kuna tatizo la kupata nafasi hizo. Je, Serikali inafikiriaje kuwapa fursa ya kuongeza muda angalau mfupi wale Askari waliostaafu badala ya kupoteza nguvu za kuajiri Askari wapya na kuwaelimisha upya wakati wale wameshakuwa na maarifa ya kazi waliyoifanya kwa muda mrefu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi kwamba tumekuwa tukitoa miongozo mara kwa mara ya kuwashauri Watumishi pale

wanapofikia umri wa kustaafu kwa kweli ikiwezekana wapumzike na tunawatumia pale tu ambapo kwa kweli hakuna mtu wa kushika ile nafasi ya yule mtu ambaye anastaafu.

Sasa kwa upande wa wa Majeshi yetu, kwanza ningependa kujibu kwamba kwanza Majeshi si Watumishi wa Umma na wenyewe wanaendeshwa kwa masharti yao ambayo suala la umri ni kigezo kikubwa sana cha mtumishi kuwepo katika ajira katika majeshi yetu.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, wastaafu wengi mara nyingi wakienda kufuatilia madai yao, huambiwa mafaili yamepotea na kama yamepotea, je, haki iko wapi na watafuatilia wapi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema wakati nikijibu swali namba mbili kwa siku ya leo kwamba Mheshimiwa Rais amepewa uwezo wa kusamehe baadhi ya masharti ambayo yanamuwezesha mtumishi kupata pensheni yake. Mojawapo ni kwamba kuna vigezo muhimu au viambatanisho muhimu vinavyohitajika ambavyo labda vimepotea. Kwa hiyo, kinachotakiwa kwa yule mwajiriwa kwanza ni yeye pamoja na mwajiri wake kujiridhisha kama yeye kweli alikuwa ni mtumishi na amefikia umri wa kustaafu.

Hata hivyo, kwenye Ofisi yetu pia tunazo kumbukumbu kwa hiyo na mwajiri na yeye mwenyewe tukijiridhisha basi huwa tunampelekea maombi Mheshimiwa Rais asamehe baadhi ya vipengelele ambavyo vinatakiwa ili yule mwajiriwa au yule mstaafu aweze kupata haki yake.

Kwa hiyo, haki haipotei, tunachoomba tuwasaidie na wakati mwingine siyo vizuri mwenyewe mwajiriwa apite anahangaika kutafuta pensheni yake, ni suala la Maafisa kwenye ofisi zile ambao wanashughulikia suala hilo kwenda kufuatilia pensheni ya mhusika.

Na. 4

**Upandishaji Hadhi Barabara**

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA (K.n.y. MHE. AHMED ALLY SALUM)** aliuliza:-

Kwa kuwa Bunge lilitunga Sheria ya Barabara Na.8 ya mwaka 2007 ili kuboresha shughuli za barabara nchini ikiwa ni pamoja na kupandisha hadhi baadhi ya barabara za Halmashauri kuwa za Mkoa na kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini imeshapeleka maombi ya kupandishwa hadhi barabara hizo kuipunguzia Halmashauri hiyo mzigo ili iweze kuzikarabati barabara nyingine vizuri zaidi:-

(a) Je, ni lini barabara ya Dindi – Solwa na Imenya – Ishinabulandi zitapandishwa daraja?

(b) Je, ni sababu zipi zinazosababisha kuchelewa kupandishwa hadhi kwa barabara hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Solwa, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haina kigugumizi chochote katika zoezi zima la kupandisha na kushusha daraja barabara kulingana na Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007. Vigezo vya kupandisha daraja barabara mbalimbali, vimeainishwa katika Sheria ya Barabara niliyokwishaitaja.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Wizara inaandaa Kanuni za Sheria hiyo (*regulations*) ili taratibu za kupandishwa na kuteremshwa daraja barabara yoyote uweze kuwa wazi zaidi. Kazi hii inaendelea kufanyika kwa umakini nchi nzima kufuatana na Sheria inavyoagiza na kazi hii inatarajiwa kukamilishwa ifikapo mwezi Septemba, 2008. Namwomba Mbunge pamoja na wananchi kwa ujumla watuvumilie kidogo ili tukamilishe kazi yenye uhakika zaidi kwa manufaa ya nchi yetu.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Kwa kuwa swali la Mheshimiwa Ahmed, Mbunge wa Solwa, linafanana sana na tatizo lililoko katika Jimbo la Shinyanga Mjini, naomba niulize swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa barabara ya Shinyanga Mjini mpaka Old Shinyanga mpaka Bubwiki ipo chini ya Wizara ya Miundombinu, je, ni lini barabara hii itajengwa katika kiwango cha lami angalau kwa awamu ya kwanza mpaka Old Shinyanga kwa kuwa barabara hii ndiko ambako kuna kiwanda cha nyama kilichopata mwekezaji, kuna kambi kubwa sana ya Jeshi na jamii kubwa sana?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, barabara hiyo aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge, nami nakiri kwamba ni muhimu sana na kwa kweli sote tungependa barabara zenye umuhimu wa namna hiyo ziweze kujengwa kwa kiwango chochote kile ili mradi iweze kuwa na uhakika wa kufikika.

Sasa suala ni kwamba ni lini barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami, siwezi kusema moja kwa moja ni lini kwa sababu hiyo inategemea uwezo wa Serikali kifedha lakini vilevile kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi hapa labda pengine katika kutazama upandishaji wa madaraja baada ya kupitia Sheria hii mpya hilo linaweza kuangaliwa kadri wakati utakavyoruhusu pamoja na uwezo wa Serikali kifedha.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara ni sawa na mishipa ya damu kwa binadamu na kwa kuwa barabara hizi zinazounganisha Mikoa mathalani barabara ya Njiapanda Oldiani kwenda Lalago Shinyanga inapochelewa kwa muda mrefu maana yake ni kwamba uchumi wa nchi unachelewa, je, ni nini kinafanya Serikali ichukue muda mrefu, miaka mingi kwa sababu Sheria yenyewe ya Barabara tulipitisha ndani ya Bunge hili muda mrefu, sasa ni nini kinafanya Kanuni hizi zichelewe kwa sababu Wizara ilituambia baada ya kupitisha tu Sheria watapandisha hadhi barabara hizi?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka niseme kwamba Serikali iliona umuhimu wa suala hili la barabara ndiyo maana hata ikaleta Sheria hapa Bungeni ili iweze kuziweka katika madaraja husika ili ziweze kuhudumiwa vizuri.

Sasa suala la kuchelewa, nataka kutofautiana kidogo na Mheshimiwa Mbunge kwamba Sheria hii tuliipitisha mwaka jana 2007 na kwa utaratibu ili Sheria iweze kuanza kutumika lazima iandaliwe Kanuni na taratibu za kuweza kuitumia sheria hiyo na nimesema hapa kwamba Kanuni hizi sasa hivi zimefikia mwisho, itakapofika mwezi Septemba, Kanuni zitakuwa zimekamilika lakini zoezi la maandalizi limeshaanza kwa sababu Mikoa imeshapewa taarifa ya kuainisha barabara ambazo wanafikiri zinaweza kupandishwa. Kwa hiyo, si kwamba hatujaanza kulifanyia kazi, zoezi lilikwishaanza kwa kushirikiana na Mikoa na kwa hakika baada ya kipindi hicho kukamilishwa kwa Kanuni, kazi hiyo itatekelezwa.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona.

Kwa kuwa matatizo ya barabara yanafanana karibu Mikoa yote na kwa kuwa Serikali imekubali kututengenezea barabara ya kutoka Misigiri kwenda Kiomboi Bomani kwa kiwango cha lami kwa kilomita kumi na moja tu na barabara hiyo ina urefu wa kilomita 21, je, Serikali haioni kwamba kuna kila sababu ya kuimalizia barabara hiyo iwe kwa kiwango cha lami kwa kilomita zote ishirini na moja?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kusema kwamba hata hizo kilomita kumi na moja ambazo zimeshaanza kutengenezwa kwa kiwango cha lami, tunapaswa kushukuru kwa sababu huo ni mwanzo kwa sababu kwa vyovyote vile haiwezekani hata kama barabara ina kilomita mia mbili na mmedhamiria kuijenga kwa kiwango cha lami basi mkaitengeneza ikamilike kwa kipindi kifupi sana. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba huo ni mwanzo tu, kadri uwezo wa Serikali utakavyokuwa unaendelea kuimarika, tunaweza kufikiria kumalizia na hizo kilomita zingine zilizosalia.

Na. 5

**Mikoa Iliyo Nyuma Kimaendeleo**

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO** aliuliza:-

Kwa kuwa Mikoa ya Kigoma, Rukwa, Lindi na Mtwara ambayo kwa sababu mbalimbali zikiwemo za kihistoria na za kiutawala, imebaki nyuma kimaendeleo na kusababisha simanzi, manung'uniko na hata hisia za kiubaguzi kwa wananchi wa maeneo hayo:-

Je, Serikali haioni kwamba, sasa ni wakati muafaka kwa Mikoa hiyo kupewa upendeleo maalumu kwenye bajeti za sekta za elimu, barabara, nishati na utawala ili ilingane au ikaribiane na Mikoa mingine?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Nicodem Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, dhana ya Mikoa iliyo nyuma kimaendeleo, imekuwa ikitumika hususani Mikoa ambayo ina miundombinu duni kama vile barabara na umeme na pia huduma za jamii kama shule na zahanati chache. Baadhi ya Mikoa hiyo ni Kigoma, Rukwa, Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za makusudi ikiwa ni pamoja na kuongeza viwango vya fedha vinavyotolewa kwa Mikoa hiyo kwenye bajeti za Serikali kila mwaka ili kuongeza kasi ya maendeleo ya Mikoa hiyo. Utaratibu huu wa kutoa upendeleo maalum kwa Mikoa hii na kwa Halmashauri zake zote umekuwa ukitumika na kuzingatiwa na Serikali.

Mheshimiwa S pika, kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2007/2008, Bajeti ya Maendeleo ya Mkoa wa Kigoma iliongezwa zaidi ya mara 3.50 kufikia TSh. 12,279,414,000/= kutoka TSh. 3,436,800,000/= zilizotengwa kwa mwaka 2006/2007; ongezeko la TSh. 8.842,614,000/=.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Maendeleo ya Mkoa wa Lindi iliongezwa kwa zaidi ya mara 8.40 kutoka TSh. 1,831,204,000/= mwaka 2006/2007 hadi TSh. 15,299,367,000/= kwa mwaka 2007/2008; ongezeko la TSh. 13,468,163,000/=.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua kama hizo, katika mwaka wa fedha 2006/007, kwa makusudi kabisa, Serikali ilitoa TSh. 200,000,000/= kwa kila Mkoa wa Kigoma, Ruvuma, Rukwa, Mtwara na Lindi kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua na kuzingatia umuhimu wa kuongeza kasi ya maendeleo kwenye baadhi ya Mikoa ya nchi yetu, katika bajeti ya mwaka 2007/2008, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa hospitali za Mikoa kumi na moja ikiwa ni pamoja na Mikoa hiyo iliyotajwa ambapo zilitengwa TSh. 600,000,000/= kila Mkoa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa hakuna Mkoa uliokamilika kwa kuwa na maendeleo ya kutosha na ya kuridhisha na pia kwamba kasi ya kujiletea maendeleo haikulingana Mkoa hadi Mkoa. Lengo la Serikali ni kuhakikikisha kuwa hakuna Mikoa ambayo inaachwa nyuma kwenye jitihada zetu za kukuza uchumi na kujiletea maendeleo.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake safi ambaye yamenipa matumaini lakini nina swali dogo tu la nyongeza.

Miradi mingi ya maendeleo katika Mikoa hii niliyoitaja hususani Mkoa wa Kigoma, imekuwa zaidi na zaidi ikitegemea fedha za wafadhili kama ambavyo yeye mwenyewe amekiri kwamba ni kweli uduni huo unahusishwa na miundombinu, nishati na kadhalika. Miradi mingi katika Mkoa wa Kigoma ambayo tunaitarajia ni ile ambayo inategemea wahisani, ambao kwa hakika utegemezi huo hauaminiki kwa asilimia mia moja. Sasa nilitaka kujua je, mkakati wa kutumia fedha zetu za ndani kwa miradi ya maendeleo kama vile nishati na barabara, Wizara ya Fedha inasemaje?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba bajeti yetu ya Serikali kwa ujumla wake inategemea misaada kutoka nje na kwa hiyo siyo suala la ajabu kwamba katika miradi ya maendeleo ya Jimbo la Kasulu pia kutakuwa na sehemu ya misaada hiyo kutoka nje. Hili jambo linatusumbua na linapaswa kutusumbua na ndiyo maana moja ya makusudi yetu ya Serikali ni kupunguza utegemezi huo na pale tutapokuwa tumepunguza, basi tutakuwa tumeweza kupeleka fedha zetu za ndani kwenye miradi ya maendeleo. Naamini kwamba tunakwenda vizuri, dhamira ya Serikali ndiyo hiyo na imani yangu ni kwamba miaka michache kutoka sasa tutaondokana na hiyo adha angalau kwa kiasi kikubwa.

**SPIKA:** Muda hautoshi na swali hili ni pana sana, mtaendelea kuliuliza baadaye. Wizara hiyo hiyo swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo ndiyo linalofuata.

Na. 6

**Viwango Vidogo vya Pensheni**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa viwango vya pensheni wanayolipwa wastaafu wengi ni vidogo sana na hali ya maisha inazidi kupanda siku hadi siku na kwa kuwa viwango vya mishahara huongezeka mara kwa mara kwa wafanyakazi wote nchini kutokana na kupanda kwa hali ya maisha:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa bila kupandisha viwango vya pensheni, wastaafu wetu watashindwa kumudu maisha yao?

(b) Je, kwa nini pensheni hiyo isiwe inabadilika kulingana na kubadilika kwa thamani ya dola kila mwanzoni mwa mwaka husika?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kutokana na gharama ya maisha kuzidi kubadilika siku hadi siku, kuna uwezekano mkubwa kuwa wastaafu wetu watashindwa kumudu gharama za maisha yao kutokana na viwango vidogo vya pensheni. Hivyo, Serikali inaendelea na jitihada ya kuona uwezekano wa kurekebisha viwango hivyo vya pensheni ili vilingane na kuongezeka kwa gharama za maisha ili kujaribu kuboresha maisha ya wastaafu.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaangalia namna endelevu ya kurekebisha pensheni ya kila mwezi kwa wastaafu. Vianzio na vigezo ambavyo vinafaa kutumika ni vile ambavyo na vyenyewe havibadiliki badiliki mara kwa mara. Hata hivyo, uwezo wa Serikali wa kulipa pensheni hizo, ni lazima utazingatiwa.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa wastaafu hawa walifanya kazi kwa uadilifu mkubwa na kwa kuwa wanasahaulika kubadilishiwa pensheni zao na kushindwa kumudu maisha pamoja na mkakati mzuri wa Serikali wa kutazama malipo haya upya, je, Serikali haioni kwamba kuna kila sababu ya kuyafanyia uthamini malipo haya kila wakati wa bajeti unapofika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa kuwa shilingi ya Tanzania hushuka mara kwa mara je, Serikali haioni kwamba kuna kila sababu sasa kulipa malipo ya wastaafu kwa kutumia dola? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kwanza kwamba ongezeko la pensheni liwekwe kwenye bajeti ya Serikali, tayari pensheni zenyewe zinalipwa kutokana na bajeti ya Serikali na ongezeko kama litakuwepo na kama nilivyosema, tunatazama jinsi ya kuongeza, basi litakuwa kwenye bajeti hiyo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu pensheni iwekewe kianzio ama ilipwe kulingana na dola, kwanza dola ni fedha ya nchi nyingine na siyo sarafu ya Tanzania lakini la pili na dola yenyewe inayumba sana.

Uchumi wa dunia sasa hivi uko kwenye hali mbaya kwa sababu ya kuyumba kwa dola na kwa hiyo nafikiri si jambo jema kutumia dola katika kurekebisha pensheni ya wastaafu.

Mheshimiwa Spika, kuna njia nyingine ambazo tunatazama, kuna njia ya kitaalamu inaitwa *indexation* lakini hilo ni moja tu kati ya mambo ambayo tunatazama. Sasa hivi tunatazama vilevile uwezekano wa kurekebisha kima cha chini cha wastaafu cha pensheni ya Sh. 21,601/= kwa asilimia fulani lakini tunachokuta ni kwamba kwa mfano, ukirekebisha kwa asilimia hamsini tu kiasi cha fedha unachohitaji ni zaidi ya Sh. 15bn/=.

Tunaelewa kwamba ni muhimu kuwatunza wastaafu wetu na kwa hiyo pamoja na kwamba hizo Sh. 15bn/= ni nyingi hiyo si sababu, sababu ni kuwa na utaratibu ambao utamwezesha huyu mwananchi ambaye alitumikia nchi yetu kwa miaka mingi na kwa uaminifu mkubwa aweze kumudu maisha yake.

Na. 7

**Tatizo la Utapiamlo Nchini**

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania ni moja kati ya nchi 20 duniani zinazoongoza kwa tatizo la utapiamlo ambapo asilimia 50 ya akina mama wana upungufu wa damu (*anaemia)* na asilimia 52 ya watoto chini ya miaka mitano wana utapiamlo wa aina mbalimbali:-

Je, Serikali inalikabili vipi tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika katika kusimamia lishe ya watoto wachanga na wadogo Serikali imeweka mikakati ifuatayo:-

- Kuzuia watoto kuzaliwa na uzito pungufu kwa kuelimisha kina mama kuhusu umuhimu wa kula vyakula vya kutosha na vya mchanganyiko wakati wakiwa wajawazito.

- Kupitisha sheria ndogo inayosimamia uuzaji wa maziwa mbadala na vyakula vya watoto wachanga *(The National Regulation on Marketing of Breast Milk Substitute and*

*Designated Products 1994).* Ikiwa ni uridhiaji wa Kanuni ya Kimataifa *(International Code on Marketing of Breast Milk Substitutes*).

- Uandaaji wa mkakati wa Kitaifa unaosimamia lishe ya watoto wachanga na wadogo uliopitishwa mwaka 2004 ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Kanuni ya Kimataifa.

- Kutoa elimu na mafunzo juu ya ulishaji wa watoto, ikiwemo unyonyeshaji wa maziwa ya mama na kumpatia mtoto vyakula vya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika kutatua tatizo la upungufu wa damu, Serikali kupitia Taasisi ya Chakula na Lishe, imeandaa miongozo mbalimbali ya lishe na kutoa ushauri na mafunzo ya jinsi ya kuzuia na kutatua tatizo hili kama vile Mwongozo wa Kudhibiti Upungufu wa Vitamini na Madini *(Policy Guideline on Supplementation*) unaotoa maelekezo ya jinsi ya kutoa vitamini na madini ya nyongeza ya vitamini ya *folic acid* na madini chuma.

Mheshimiwa Spika, juhudi hizi za Serikali zimeleta mafanikio kwa kiasi kikubwa.

- Zaidi ya asilimia tisini ya watoto wa umri chini ya miaka mitano nchini wanapata matone ya vitamini A na dawa za minyoo kila baada ya miezi sita.

- Viwango vya utapiamlo vimepungua ambapo udumavu umepungua toka asilimia nne mwaka 1992 mpaka asilimia arobaini na nne mwaka 1999 na baadaye mpaka asilimia thelathini na nane mwaka 2004; ukondefu umepungua toka asilimia tano nukta sita mwaka 1992 mpaka asilimia tano mwaka 1999 na baadaye asilimia tatu mwaka 2004.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Kwa kuwa moja ya sababu kubwa inayochangia utapiamlo ni pamoja na umaskini uliokithiri hasa miongoni mwa akina mama, je, ni kwa nini Wizara isishirikiane na Wizara husika pamoja na wadau mbalimbali ili kuhakikisha kwamba inawapatia akinamama hawa mafunzo ya ujasiriamali pamoja na mikopo?

(b) Kwa kuwa pamoja na kupelekea udumavu wa kimwili, tatizo la utapiamlo pia hupelekea matatizo ya udumavu wa kiakili hasa kwa watoto hawa ambao wapo chini ya umri wa miaka mitano, je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kupunguza tatizo hili la udumavu wa akili kwa watoto hawa wenye utapiamlo?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, ni kweli kabisa umaskini uliokithiri ndio unaosababisha watoto hawa

wasiweze kupata lishe bora na hivyo kuna umuhimu wa kuwawezesha akina mama kuweza kujipatia kipato na hivyo kujipunguzia umaskini.

Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kweli kwamba Wizara kupitia Taasisi ya Chakula na Lishe kutoa elimu na kuweza kuwafundisha akina mama jinsi ya kuandaa vyakula ambavyo wanavipata katika maeneo husika hasa wakati wanapoasili watoto.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu udumavu, ni kweli kabisa udumavu wa akili unapelekea watoto kutomudu vizuri katika masuala ya elimu hivyo kuongeza umaskini katika maisha ya Watanzania. Wizara yangu kwa kushirikiana na taasisi husika, tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi na hasa kuwaambia akina mama wanapokuja kliniki kuhakikisha kwamba watoto kwanza wananyonyeshwa ziwa la mama wanapozaliwa na kuzingatia maelekezo wanayopewa katika vituo vya afya ili kuhakikisha kwamba chakula wanachowapa kinakidhi na hivyo kupunguza udumavu wa akili na hatimaye watoto waweze kumudu masomo wanapokuwa darasani.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, nitaongeza muda kidogo kwa sababu tulianzia na Wimbo wa Taifa na matangazo mengine. Kwa hiyo, tutaendelea nayo kidogo. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Viti Maalum.

Na. 8

**Ugonjwa wa Akili Kuongezeka**

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH** aliuliza:-

Kwa kuwa kwenye siku za hivi karibuni kumekuwepo na ongezeko kubwa la wagonjwa wa akili hapa nchini:-

(a) Je, Serikali itakuwa tayari kueleza ni sababu gani zinazosababisha ugonjwa wa akili hapa Tanzania na ni sababu zipi zinaoongoza?

(b) Je, kuna hospitali ngapi zinazotibu ugonjwa huo hapa nchini na upatikanaji wa dawa kwa wagonjwa hao ukoje?

(c) Je, nini kinga ya ugonjwa huo wa akili?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, zipo sababu nyingi zinazosababisha ugonjwa wa akili hapa Tanzania. Baadhi ya sababu hizo ni kama ifuatavyo: Kurithi kutoka kwa vizazi vilivyotangulia; hali mbaya ya kimaisha inayoleta umaskini; uhusiano mbaya wa kifamilia na kijamii; matumizi ya pombe kupita kiasi; matumizi ya dawa za kulevya; na magonjwa kama vile malaria na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu zinazotokana na mahudhurio katika kliniki za wagonjwa wa akili; sababu zinazoongoza kusababisha ugonjwa wa akili ni matumizi ya pombe kupita kiasi; matumizi ya dawa za kulevya; na uhusiano mbaya wa kifamilia unaosababisha msongo wa mawazo.

(b) Mheshimiwa Spika, hospitali maalum kwa ajili ya huduma ya matibabu ya magonjwa ya akili hapa Tanzania ni Hospitali ya Mirembe, iliyopo hapa Dodoma na Hospitali ya Lutindi iliyoko Wilaya ya Korogwe, Mkoa wa Tanga. Aidha, Hospitali za Mikoa ya Dar es Salaam, Iringa, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Ruvuma na Tabora, zina vitengo maalum vya kuhudumia wagonjwa wa akili. Azma ya Serikali ni kuhakikisha hospitali zote za Mikoa na Wilaya, zinakuwa vitengo maalum vya kuhudumia wagonjwa wa akili.

Dawa muhimu za kifafa na magonjwa sugu ya akili, zinapatikana na zinawafikia wagonjwa wengi. Vituo vya kutolea huduma vinatakiwa kuandaa takwimu za mahitaji ya dawa na kuwasilisha *MSD* ili dawa hizo ziagizwe kwa wingi zaidi.

(c) Mheshimiwa Spika, kinga dhidi ya magonjwa ya akili ni kama ifuatavyo: Kuepuka ulevi wa kupindukia; kuepuka matumizi ya dawa za kulevya; kula vizuri, yaani mlo kamili; iwapo upande mmoja wa wanandoa una historia ya ugonjwa wa akili ni vyema kutafuta ushauri wa madaktari kuhusu jinsi ya kuepuka tatizo hilo; kujitahidi kuepuka mazingira yanayoweza kusababisha msongo wa mawazo; na kujitahidi kuepuka baadhi ya magonjwa ya kuambukiza kama vile Malaria na UKIMWI, yanayoweza kusababisha ugonjwa wa akili ikiwa hayatatibiwa ipasavyo.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kuna wagonjwa wengine wa akili wanatumia dawa kwa muda fulani na baadaye wanasita kuzitumia na wanakaa muda mrefu hawajaugua mpaka wanajamii na wana ndugu wanawaona kama hao wamekwishapona; pengine miaka mitano mpaka kumi, lakini baadaye ugonjwa unalipuka tena; je, ni kusema ugonjwa huo hauna dawa?

La pili ni kwamba, kuna wanawake wengine wanasimama hadharani na kuwatukana waume zao matusi ya nguoni; kinyume na maadili na taratibu za jamii Fulani; na waume nao huwatukana wake zao vilevile; je, hii ni aina gani ya ugonjwa wa akili? Ahsante. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Majibu Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, lakini miongoni mwa hao, bahati nzuri Waheshimiwa Wabunge hawahusiki. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ni kweli kabisa kuna baadhi ya wagonjwa, baada ya kutumia dawa kwa muda mrefu, ile hali ya kuwa na matatizo huwa inakwisha kabisa, lakini baadaye inarudi tena.

Mheshimiwa Spika, sababu zipo nyingi; kwanza, inawezekana kwamba, kuna magonjwa mengine ya ugonjwa wa akili huwa hayatibiki kabisa, lakini huwa yanaweza yakawa yamepungua kwa muda mrefu. Endapo sababu za kupata ugonjwa wa akili ni pombe na kama aliacha na baadaye akarudia tena, hii inaweza ikawa ni sababu ya ugonjwa ule kurudia tena. Kwa hiyo, inategemea sababu ya kupata ugonjwa ule ni nini na kama atakuwa amerudia, basi inawezekana ikajirudia ile hali.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la wanawake kuwatukana waume zao na wanaume kuwatukana wake zao, kuna mawili; inaweza ikawa ni tatizo la ugonjwa wa akili, lakini inawezekana kwamba ni tabia mbaya tu ambayo wanawake na wanaume wamejijengea, katika maadili mazima ya maisha.

Kwa hiyo, kutukana siyo lazima uwe ni ugonjwa, lakini kutukana inawezekana ni tabia mbaya tu ambayo watu wanayo. Kwa sababu haiwezekani mtu mwenye busara, akasimama nje hadharani akaanza kutukana, hata kama hamtukani mkewe au mumewe, lakini kutukana kama tendo la kutukana, siyo tabia nzuri na wala haihusiani saa nyingine na kwamba ana ugonjwa wa akili, ila ni tabia mbaya. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumalizie sasa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, swali linalofuata lilikuwa liulizwe na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, alimwachia Mheshimiwa Josephine Genzabuke aliulize.

Na. 9

**Uhaba wa Walimu kwa Shule za Sekondari**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE (K.n.y. MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI)** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wengi wa Wilaya ya Kasulu wamefanya kazi kubwa ya ujenzi wa Shule za Sekondari; na kwa kuwa tatizo kubwa linalowakabili ni uhaba wa walimu na vitendea kazi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka walimu wa kutosha kwenye shule hizo?

(b) Je, Serikali ina mpango wowote wa kufungua shule za Sekondari za Kidato cha Tano na Sita na kuanzisha Vyuo vya Ufundi ili kuwasaidia wanaomaliza masomo kwenye shule hizo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kilontsi Muhama Mporogonyi, Mbunge wa Kasulu Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu upungufu wa walimu uliopo katika Wilaya ya Kasulu na Mkoa wa Kigoma kwa ujumla. Wilaya hiyo ina jumla ya walimu 214 wa Shule za Sekondari na inao upungufu wa walimu 265. Katika mwaka 2007/2008, Wizara iliwapanga walimu 95 katika Wilaya ya Kasulu; kati ya hao walimu18 hawakuripoti. Kutokana na uhaba mkubwa wa walimu uliopo nchini, Wizara yangu inatekeleza Mpango Kabambe wa Mafunzo ya Walimu ili kukidhi mahitaji ya walimu wa shule za msingi na sekondari kwa nchi nzima ifikapo mwaka 2012/2013. Mpango huo unatekelezwa kwa kuongeza nafasi za kusomea Ualimu kwa Ngazi ya Cheti, Stashahada na Shahada.

Katika mwaka wa 2007/2008, walimu watakaohitimu na kupangiwa kufundisha Shule za Sekondari (Ngazi ya Stashahada ni 5,959 na Shahada ni 2,843). Walimu hao wataajiriwa wote na kupangwa katika Shule za Sekondari, ikiwa ni pamoja na shule za Wilaya ya Kasulu. Wananchi kwa kushirikiana na Halmashauri zao, waendelee kuandaa mapokezi mazuri kwa walimu wapya, wanaopangwa katika Mikoa na Wilaya, ikiwa ni pamoja na kujenga nyumba za kuishi walimu hao.

(b) Mheshimiwa Spika, baada ya upanuzi mkubwa wa Shule za Sekondari kwa kidato cha kwanza hadi cha nne, vijana waliomaliza Elimu ya Sekondari kwa nchi nzima wamaeongezeka kutoka 77,238 mwaka 2005 na kufikia 115,302 mwaka 2007 na wanaotegemewa kuongezeka kufikia 326,935 mwaka 2010. Changamoto kubwa iliyo mbele yetu ni kupanua Elimu ya Sekondari katika kiwango cha kidato cha tano na Sita kwa nchi nzima. Hatua mbalimbali zitachukuliwa, ikiwa ni pamoja na kila Wilaya kutayarisha shule mbili za Kitaifa, zenye mikondo mitatu kwa Kidato cha tano na mitatu kidato cha sita. Shule hizo zitapokea wasichana katika shule moja na wavulana katika shule ya pili. Aidha, shule chache za Kata zitakazokidhi vigezo, zitaongezewa hadhi kuwa na kidato cha tano na sita. Katika mwaka 2009, Serikali itaanza kuzibadilisha hatua kwa hatua, shule zote za bweni za Serikali kuwa na kidato cha tano na sita pekee. Lengo ni kufikia wanafunzi 120,000, kuweza kupata nafasi za kidato cha tano ifikapo mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeandaa Mpango wa Kuviimarisha Vyuo vya Ufundi vya *VETA* vya Mikoa na baadaye vya Wilaya, ili viweze kutoa mafunzo katika *level one* hadi nne, kwa lengo la kuwachukua wanaomaliza masomo kwenye shule za sekondari, ambao hawatapata nafasi ya kujiunga na kidato cha tano.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Kwa kuwa kwa muda mrefu imedhihirika kuwa walimu wanaopangwa katika Mkoa wa Kigoma huwa wanakataa kwenda Mkoani Kigoma kutokana na miundombinu mibovu inayouathiri Mkoa huo; je, Wizara inaweza kutufanyia mpango maalum wa kuwafundisha walimu kwa wingi ili waweze kuja kuusaidia Mkoa wa Kigoma?
(b) Je, Serikali inawachukulia hatua gani walimu wanaopangiwa kuripoti Mkoa wa Kigoma halafu wanakataa kwenda?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Spika, walimu kutoenda katika Mkoa wa Kigoma, inawezekana kuna sababu nyingi kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, lakini kama tulivyoshauri, Mikoa yote na Wilaya zote, walimu watakaopangwa wajiandae kuwapokea kwa kuwatafutia miundombinu kwa mfano, nyumba za kuishi na mazingira mazuri kwa ujumla ya kuishi.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Rukwa ni mfano mzuri sana wa kupokea walimu wageni. Wana Mfuko wao na ule Mfuko unafanya kazi ya ziada, ambayo Wizara na Serikali kwa ujumla, haiwezi kufanya ikiwa ni pamoja na kuwapa fedha za kujikimu, kuwapatia nyumba na kuwapatia usafiri wanaporipoti kutoka katika Ofisi za Wilaya hadi kwenye Shule. Wito wangu na wito kwa ujumla wa Wizara ni kwamba, waige Mkoa wa Rukwa na wautembelee Mkoa wa Rukwa, wajaribu kujifunza wanachofanya ili kuwavutia walimu wao waende kufundisha katika Mkoa ule, ambao zamani kila mtu alikuwa hataki kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la (b), hatua gani tunachukua; hatuwezi kumchukulia mwalimu hatua kabla hatujamwajiri, hana *EDF* na hatumfahamu. Kwa hiyo, mpaka anapoajiriwa ndipo tunapomchukulia hatua, kama akishindwa kuhama kutoka kituo kimoja kwenda kingine. Tunaomba tusaidieni hasa tunapokuwa tunawapanga walimu, Waheshimiwa Wabunge njooni mchukueni majina ya walimu wale muwafuatilie ili waweze kuripoti katika maeneo waliyopangiwa na wawaahidi kwamba, watawasaidia kuwa na mazingira mazuri, zikiwemo nyumba za kuishi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali la mwisho, Wizara hiyo hiyo, linaulizwa na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani.

Mheshimiwa Mbunge, hukusikika umenong'ona, lakini hali yako ni salama?

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nipo salama.

**SPIKA:** Ahsante sana, nashukuru.

Na. 10

## Vurugu na Migomo ya Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu Nchini

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwepo na ongezeko kubwa la vurugu na migomo ya wanafunzi katika Vyuo vya Elimu ya Juu hapa Nchini na kutishia hali ya amani na utulivu katika maeneo husika:-

(a) Je, Serikali inafanya utafiti gani juu ya chanzo cha vurugu na migomo hiyo?

(b) Je, hatua zinazochukuliwa kuzuia migogoro hiyo zinaleta ufumbuzi wa kudumu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na vurugu na migomo ya mara kwa mara kwa wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa kuzingatia tatizo hili, iliyokuwa Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, iliunda Tume ya Uchunguzi kuhusu vyanzo vya migomo katika Vyuo vya Elimu ya Juu ili kuishauri Serikali ipasavyo. Tume hiyo iliyoongozwa na Dr. Hawa Sinare, ilikabidhi Ripoti yake kwa Waziri mwenye dhamana ya Elimu ya Juu, tarehe 1 Juni, 2004. Tume ilitembelea Vyuo Vikuu vya Umma 7 na Chuo kimoja cha binafsi na kufanya mahojiano na wahadhiri, wafanyakazi, waendeshaji na wanafunzi.

(b) Kwa ujumla, Ripoti ilibaini vyanzo muhimu vya migogoro kama vile ucheleweshaji wa mikopo ya wanafunzi, upungufu wa fedha kwa ajili ya aina zote za mafunzo kwa vitendo, upungufu wa bajeti ya maendeleo, upungufu wa nafasi hasa za mabweni, madarasa, maktaba, karakana, maabara na uongozi duni katika baadhi ya Vyuo vya Elimu ya Juu, kushindwa kugundua matukio ambayo yangeweza kutafutiwa ufumbuzi kwa wakati. Katika Vyuo Vikuu vingi, mabweni yapo katika hali mbaya sana; kwa mfano, kukosa maji, umeme, milango, madirisha na kuwa na samani zilizoharibika kabisa.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali imeshaanza kuyafanyia kazi, baadhi ya mapendekezo ya Tume tajwa na itaendelea kuziimarisha Taasisi za Elimu ya Juu ili kuepuka vurugu na migogoro ya wanafunzi. Kwa mfano, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, imeimarishwa kwa kuajiri watumishi wa kutosha na wenye sifa, imenunua vitendea kazi bora, imewekwa mfumo wa kitaalamu wa kutambua uwezo wa kiuchumi wa mwombaji mkopo.

Maeneo mengine yaliyofanyiwa kazi ni pamoja na kufanya ukarabati katika Taasisi zote za Elimu ya Juu za Umma na kuongeza mabweni, kumbi za mihadhara na madarasa.

(b) Mheshimiwa Spika, hatua zinazochukuliwa kuzuia migogoro katika Vyuo vya Elimu ya Juu zinaleta utatuzi wa kudumu, lakini ambao hauwezi kuonekana katika muda mfupi. Migogoro inayosababishwa na udhaifu wa mawasiliano kati ya Uongozi wa Vyuo na Jumuia ya Wanafunzi, ufumbuzi wake unaweza kupatikana haraka. Migogoro inayotokana na uhaba wa ruzuku kwa vyuo au viwango vidogo vya posho/mikopo kulingana na bei na soko, itatatuliwa kadiri hali ya bajeti itavyokuwa nzuri.

Aidha, Wizara yangu itazidi kuimarisha safu za uongozi wa Taasisi za Elimu ya Juu hasa za umma, kuimarisha Bodi ya Mikopo na kuendelea kuwaelimisha wanafunzi juu ya wajibu wao na njia rasmi za kuwasilisha malalamiko waliyonao kwa vyombo vinavyohusika.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali madogo ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa uzoefu unaonyesha kuwa miongoni mwa vyanzo vikuu vya vurugu na migomo ya wanafunzi vinatokana na Wakuu wa Vyuo hivyo kutosikiliza ka upeo matatizo ya wanafunzi hao; badala yake wanafunzi wanapogoma wanafukuzwa na wanapofukuzwa walimu wanakosa kaz halafu wanafunzi wanaitwa warudi Vyuoni na husababisha hasara kubwa kwa Taifa; je, Serikali inawachukulia hatua gani ya kinidhamu au ya kisheria; Wakuu wa Vyuo hivyo ambao wanasababisha hasara kubwa kwa Taifa, ambayo ni aina nyingine ya ufisadi? *(Makofi)*

La pili, kwa kuwa hivi karibuni katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakati wa mgomo, baadhi ya wanafunzi walijeruhiwa na Jeshi la Polisi ambalo lilipelekwa hapo kwa ajili ya kuzuia mgomo; je, Serikali ilishindwa kutumia busara na hekima na mbinu za kisayansi, kutuliza migomo ya wanafunzi, badala yake inapeleka Jeshi la Polisi ambalo kazi yake ni kutumia mabavu tu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Spika, uzembe wa Wakuu wa Vyuo au Manaibu Wakuu wa Vyuo, siyo sababu pekee inayosababisha migomo Chuoni. Nimeeleza katika jibu langu la msingi, baadhi ya mambo yanayochangia ikiwemo miundombinu isiyoridhisha, yakiwemo maji ambayo ni nje ya uwezo wa Taasisi yenyewe. Hadi sasa, Wizara yangu haijabaini mahali ambapo Mkuu wa Chuo peke yake amesababisha uzembe huu na hivyo kuweza kumchukulia hatua za kidhamu. Mara nyingi tunakutana na tunazungumza, tukibaini matatizo tunashauriana jinsi ya kuyatatua na mara nyingi Vyuo vyenyewe vinafanya hivyo.

Kwa upande wa swali la pili, hakuna mwanafunzi aliyejeruhiwa na Polisi isipokuwa wanafunzi walimjeruhi Polisi.

Mheshimiwa Spika, inapotokea fujo yoyote, hata ikitokea humu ndani, utaita Polisi hutaweza kutatua tatizo ambalo kweli linahitaji nguvu ya pekee na chombo pekee cha Kiserikali, kinachoshughulikia masuala hayo ni Jeshi la Polisi. Kwa hiyo, tutaendelea kutumia Jeshi la Polisi katika Vyuo vyetu na wengi mnajua vurugu zinapotokea katika Vyuo vile, wanafunzi wanaumizana na hakuna mwingine anayeruhusiwa na mwenye uwezo na mwenye utaalam wa kushughulikia fujo kama hizo isipokuwa Polisi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita kabisa, ingawa tumeweza kumaliza maswali yote kumi. Tuna matangazo yafuatayo:-

Waheshimiwa Wabunge, natangaza wageni wa Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mzee Johnson Bakila na Mama Marynasi Bakila, hawa ni wazazi wa Mheshimiwa Mbunge. Wazee naomba tafadhali msimame tuwatambue.

*(Hapa wazee waliotajwa walisimama)*

**SPIKA:** Wale pale, karibuni sana. Ahsanteni sana na pole kwa safari ndefu.

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wanafunzi wanane wa Chuo cha Ardhi Morogoro. Wanafunzi wa Chuo cha Ardhi naomba wasimame.

*(Hapa wanafunzi waliotajwa walisimama)*

**SPIKA:** Wale pale, ahsante sana na karibuni sana. Tunawatakia mema katika mafunzo yenu.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu mikutano; Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, anawaomba leo hii saa 05.00 asubuhi, Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane Ukumbi Namba 231 katika Jengo la Utawala.

Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, *Chief Whip* wa Upinzani, ameomba nitangaze kwamba, Waheshimiwa Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani, wakutane leo mara baada ya shughuli hizi za asubuhi.

Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Katibu wa Kamati ya Wabunge wa CCM, ameniomba nitangaze kwamba, leo saa 05.00 asubuhi, Wajumbe wote Kamati ya Uongozi ya Chama cha Mapinduzi wakutane katika Ukumbi Namba 118.

Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Katibu wa Kamati ya Wabunge wa CCM, ameniomba nitangaze kwamba, leo saa 11.00 jioni, Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi, wakutane katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge wote wa Vyama vya Upinzani, watakutana katika Ukumbi wa Chifu Kasusura, nilisahau kusema hilo.

Waheshimiwa Wabunge, tunao utaratibu wa kuwatambua wenzetu, ambao wamefanya vizuri sehemu yoyote ambapo tumewatuma. Sasa leo kwa furaha, ninapenda kutangaza kwamba, Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Alhaj Athumani Janguo, kule katika Bunge la Afrika, ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi Vijijini, Kilimo, Maliasili na Mazingira. Ningeomba asimame.

*(Hapa Mhe. Athumani S. Janguo alisimama)*

**SPIKA:** Kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge, tunapenda kukupongeza sana Mheshimiwa Athumani Janguo. Tunajua umekuwa ni msaada sana ndani ya Bunge na sasa hata Bunge la Afrika limeweza kukutambua. Tunajivuna sana kwa hilo. Hongera sana. *(Makofi)*

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, ninaruhusiwa kusema maneno mawili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, bado ngoja nimalize matangazo.

Waheshimiwa Wabunge, kesho baada ya kipindi cha maswali, tutakuwa na Muswada wa *Public Audit Bill*, 2008 na Muswada huu ni muhimu sana, umeletwa na nimekwisha andikiwa hapa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba, anaomba upitishwe kwa hatua zote.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 93(1), ambayo nitaisoma, utaratibu utakuwa kama ufuatao: Kwanza, inasema: “Bunge halitashughulikia hatua zaidi ya moja, kwa Muswada wowote wa Sheria katika Mkutano mmoja wa Bunge.” 93(2) sasa: “Bila kuathiri masharti ya hiyo fasili ya (1), Bunge linaweza kushughulikia Muswada wa Sheria katika hatua zaidi ya moja, endapo hoja mahususi itatolewa kwamba, Muswada huo ushughulikiwe katika hatua zaidi ya moja. Spika ataridhika na hoja hiyo na Bunge litaafiki hoja hiyo kwa kupiga kura.”

Kwa hiyo, kesho baada ya kipindi cha maswali, nitawahoji na nadhani Muswada huu ni muhimu, baada ya hapo mkiridhia basi tutaendelea moja kwa moja. Ni matumaini yangu, kufikia jioni tutaweza kuwa tumeumaliza Muswada huo.

Waheshimiwa Wabunge, niseme moja, kuchangia katika Muswada huo, hakumpunguzii Mheshimiwa Mbunge yeyote, nafasi yake ya kuchangia katika Hotuba ya Bajeti inayofuata. Ninajua utaratibu wetu, ukichangia kwa mfano, Hotuba ya Bajeti, basi haitakuwa rahisi kuchangia kwenye Makadirio ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kadhalika na kadhalika. Muswada huu ni mahususi, ambao hauchanganyiki na hotuba za bajeti nyingine. Kwa hiyo, mkisharidhia kesho, nitaomba tu mjiamini kabisa kwa wale ambao mnataka kuchangia waweze kuchangia na hawatahesabika kwamba, wamepoteza fursa ya kuchangia katika hotuba za bajeti nyingine zinazofuata.

Sasa nimepokea ombi la Mheshimiwa Athumani Janguo, ningeomba aseme kwa kifupi. Mara nyingine huwa ninatoa ruhusa hii halafu haitumiki vizuri sana. Kwa hiyo, kifupi maana yake haizidi dakika kama mbili na nusu hivi. Mheshimiwa Athumani Janguo.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niseme maneno mawili tu. La kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ndiye aliyeniwezesha kufika katika Bunge hili na yeye akaniwezesha kufika katika Bunge la Afrika. Vilevile akaniwezesha kupata nafasi hiyo ambayo nimeipata.

La pili, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kama wasingenichagua kuingia katika Bunge la Afrika, basi nafasi hiyo nisingeipata, hususan katika mwaka wa 2005, baada ya kuwepo kule katika kipindi kilichopita na kurudi hapa, mlikuwa na uhuru wa kuweza kusema kwamba sasa hapana, lakini mkaturuhusu mimi na Mheshimiwa Dr. Getrude Mongella, halafu mkawachagua na wengine. Kwa hiyo, kwa ukarimu wenu, nasema shukrani sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niishukuru vilevile familia yangu, wao ndiyo walikuwa wakinipa nguvu wakati wowote ule na mpaka sasa hivi, kwa hiyo na wao ninawashukuru vilevile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwamba, uteuzi huu siyo wa Athumani Janguo ni wa Bunge la Tanzania na Watanzania wenyewe. Kule tupo katika Kanda Tano; kwa hiyo, katika kanda moja akipatikana kiongozi na hasa kwa Tanzania, nafasi yetu ilikuwa ndogo kwa sababu baada ya kumpata Rais wa Bunge la Afrika, basi tulikuwa hatuna nafasi tena ya kuweza kugombea kiti katika Kamati zile kumi.

Hili liliwezekana na liliwezekana kwa sababu ya nguvu ambayo ninyi Waheshimiwa Wabunge, mmekuwa mkitupa na kutushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu kubwa ni kwamba, Waheshimiwa Wabunge endeleeni kunishauri mimi na wenzangu ili tukiwa katika Bunge la Afrika, tuweze kuifanya kazi ile ambayo mmetutuma.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Athumani Janguo, ahsante sana kwa hayo. Tunakutakia kheri pamoja na wenzio.

Waheshimiwa Wabunge, shughuli ambazo zilikuwa zimepangwa kwa siku ya leo tumezikamilisha. Kwa hiyo, naliahirisha Bunge hadi kesho Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 04.30 asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 11 Juni, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*